

TAI WANAKUSANYIKA PAMOJA! Tarehe 03/10/2026. Jumamosi.

Wapendwa Akina Mikaya,

Vile vita vikuu sana vilivyowahi kupiganwa sasa viko tayari kuanza. Mungu amekuwa akiwachagua wanajeshi Wake wa hali ya juu kwa zaidi ya miaka elfu sita, nawe ulikusudiwa kimbele na kuchaguliwa kuwa katika Jeshi Lake Kuu.

Yeye amekuwa akikuvisha, na kukupa mafunzo, nao uwanja wa vita sasa umewekwa tayari, unajiandaa kuanza. Sio tu kwamba Yeye alikuchagua kuwa katika Jeshi Lake Kuu, bali Yeye amekuteua wewe kuwa Mikaya nabii katika jeshi Lake.

Wakati umefika, siku yenyewe imefika; utapokea mafunzo moja kwa moja kutoka kwa Nguzo ya Moto Mwenyewe ili kumshinda kila adui. Utapokea maagizo maalum, Neno kwa Neno, juu ya nini cha kufanya ili kuangamiza kabisa kila roho mchafu. Itaupeperusha kila ugonjwa na kila pepo anayekuja mbele yako. Hakuna kinachoweza kusimama mbele yako.

Baada ya mafunzo haya maalum, utakuwa umewekewa ngome mno kwa Neno Lake kiasi kwamba utauondoa uovu wote. Tupilia mbali hoja. Tupilia mbali ushirikina. Tupilia mbali wasiwasi. Tupilia mbali magonjwa. Tupilia mbali dhambi. Utaelewa uko juu yake, umefufuka katika Kristo Yesu, umeketi katika ulimwengu wa Roho na kila pepo akiwa chini ya miguu yako. Utaelewa kikamilifu na KUAMINI wewe ni Neno.

Yeye atawapa mafunzo ya lipi la kuwa nalo macho. Atawafundisha kwamba ikiwa adui yako anaweza kukufanya uamini Silaha yako haina nguvu vya kutosha, yeye atakupokonya silaha.

Lakini tutayakumbuka mafunzo yetu, enyi askari, na kumwambia huyo shetani: Sio sisi, sisi si kitu. Silaha yetu ni Neno la Mungu nalo litamshinda KILA PEPO, wakati wowote, mahali popote, kwa sababu ni NENO LAKE, NAYE ALITUPA MAFUNZO NA KUTUFUNULIA KWAMBA SISI SASA NI NENO LAKE LILILOFANYIKA MWILI. HIVYO, hatuwezi kushindwa, sisi ni jeshi LA MUNGU lisiloshindwa.

Moja ya siku zilizo kuu mno katika historia ya ulimwengu inaenda kutukia Jumapili hii. Akina Mikaya Wake wataungana pamoja kutoka kote ulimwenguni chini ya Sauti ya Jenerali wao mkuu, ambapo tutaungana pamoja hasa kwa nia moja, bila hata chembe moja ya shaka popote.

Kisha, ikiwa tu tutaamini, NASI TUNAAMINI, hakutakuwa na mtu dhaifu ulimwenguni kote. Ikiwa tukiweza tu kurekebisha jambo hilo fulani, hakutakuwa na mtu anayemtamani Roho Mtakatifu ila yule ambaye angempokea, nako kutakuwa na uponyaji wa ghafla wa roho na mwili, ikiwa tutashikilia tu nafasi zetu. Huu ndio wakati wenyewe. Sisi ndio watu hao. Roho wa Mungu ameinua beramu dhidi ya kila pepo; sisi ni MMOJA WAO na hakuna kinachotuzuia!!

Tumekufa kwa dhamiri zetu, tumekufa kwa hoja zetu, tumekufa kwa mambo yote hayo. Maisha yetu yamefichwa nasi tumezikwa katika Jina la Yesu Kristo, na kufufuliwa pamoja Naye. Na po pote alipo Yeye, hapo ndipo nasi tulipo pia.

Tumedonoa tukatoka, ewe shetani, kwa kukulipua kwa, "BWANA ASEMA HIVI. BWANA ASEMA HIVI. BWANA ASEMA HIVI." Hatimaye tunainusa hewa safi. "BWANA ASEMA HIVI." Sisi hawa hapa tunakuja shetani, tumetokeza vichwa vyetu nje. "BWANA ASEMA HIVI, UMESHINDWA."

Tunamshinda shetani kwa kitu gani?

Neno!

Hebu na tuseme; Neno! Neno! NENO!!

MAAGIZO ZAIDI YA MAFUNZO

Sasa wakati adui anaposhambulia na kujaribu kusema ati unapaswa kufanya hivi, unapaswa kufanya vile, wewe hufai, hustahili, hujapona, bado ungali una matatizo yako yale yale. Utafanya nini?

Ondoka kwangu." Mpige dharuba! Kisha umkate kwa Neno. Iwe ni pepo; iwe ni adui; iwe ni maradhi; iwe ni ugonjwa; cho chote kile; chukua hilo Neno ulivute kwa Upanga, na kama ukilipiga dharuba mara ya kwanza nalo halielekei kusogea, **lipige dharuba tena, na ulipige dharuba tena, na ulipige dharuba tena!**

Tunalikubali tu Neno kwa msingi wa, "Mungu alisema hivyo." na hilo linafanya kijito kati yetu na Yeye. Kila mkondo umefunguka kati yetu. Tunasema, "Sijui ni lini nitalipata, bali nitalipata. MUNGU ALISEMA HIVYO. Kila shaka IMETOWEKA...hata tunatilia shaka mashaka yetu."

Tunampinga shetani na kulichukua Neno la Mungu. Ikiwa najisikia hisi fulani, au bila hisi, haijalishi kinatokea nini, Mungu alisema hivyo. Hilo latosha.

Yafuateni maagizo haya, enyi askari, kwa kina. Yarudieni Maneno haya wakati adui anaposhambulia. Si Maneno yenu, ni MANENO YAKE YEYE, NA MANENO YAKE HAYAWEZI KUSHINDWA. Yeye ametupa uwezo wa kulitumia Neno Lake kwa kutufanya sisi kuwa Neno Lake. Wakati Shetani anaposhambulia, msomeeni maagizo yenu.

MAAGIZO YA JENERALI WETU

Hiki ndicho hasa ninachowataka mfanye.

Rudia kiapo hiki na uamini kila Neno kwa ajili ya ukombozi mkamilifu.

Shetani, simile; ninatoka humu ndani; silali hapa tena; sikai hapa tena; siko kwenye ardhi hii ya ibilisi ya kale tena; ninadonoa nipate njia ya kutoka asubuhi hii! Amina! Mimi ni tai!” Amina! Haleluya!

Kisha nakutaka ufanye hivi:

Kulilipua na BWANA ASEMA HIVI. BWANA ASEMA HIVI. BWANA ASEMA HIVI.”
Fungua akili yako, useme, “Neno Lako ni Kweli.”

Bwana, sitajali jinsi ninavyojisikia, jambo mtu mwingine asemalo; ninafunga, ninasafisha kila moja ya njia zangu. Mahangaiko yote, na mashaka, na kutokuamini ambako nimepata kuwa nako; kila kuhisi ulikowahi kuwa nako; maradhi yote niliyowahi kuwa nayo; kila kitu kingine nilichopata kuwa nacho; ninavitupilia vyote nje; ninavipuuza vyote na kuja moja kwa moja kwa Roho yangu.

IMANI yako itaanza kupanda juu zaidi na zaidi. Kisha mwambie Yeye, “Ee Bwana, shuka; Wewe ulisema, Wewe ulinifanya mimi mtu mwenye hiari.”

“Ndivyo ulivyo, Mwanangu.”

Sawa, ninafungua moyo wangu na akili yangu.

“Karibu, Bwana Yesu.”

Uinyakue ile imani, Upanga wa Roho, BWANA ASEMA HIVI!

Piga kelele, Haleluya! Amina!

Kisha katilia mbali kila adui aliye mbele yako. Amina. Jambo ndilo hilo. Kata kila adui. Iwapo pe—pepo mchafu wa kale anakufanya ujisikie...Katilia mbali kitu hicho kwa Neno la Bwana.

MAAGIZO YAKO YA MWISHO EWE ASKARI.

MWAMBIE ADUI:

“Ondoka kwangu.” Mpige dharuba!

Kisha umkate kwa Neno.

Iwe ni pepo; iwe ni adui; iwe ni maradhi; iwe ni ugonjwa; cho chote kile; chukua hilo Neno ulivute kwa Upanga: na kama—kama ukilipiga dharuba mara ya kwanza nalo halielekei kusogea, lipige dharuba tena, na ulipige dharuba tena, na ulipige dharuba tena! Na ulipige dharuba mpaka umetoboa tundu, kama kifaranga mdogo akijitokeza mwenyewe nje; au tai, ndivyo ulivyo. Jitokeze moja kwa moja kutoka hilo gamba la kale la maradhi, fyeka upate njia ya

kutokea, kisha useme, “Haleluya! yuko wapi mwingine?” Amina! Hivyo ndivyo vita; huyo ndiye askari. Huyo ndiye askari wa msalaba. Ndiyo, bwana! Mtupilie nje kila adui. Kwa nini? Kwa nini?

Sisi ni Mzao wa Kifalme wa Ibrahimu uliochaguliwa tangu awali.

Utukufu, kila adui ameshindwa. Hakuna kitu CHOCHOTE kinachoweza kusimama mbele ya Neno la Mungu, nasi ni Neno la Mungu. Sisi ndio Uzao Wake wa Kifalme na kila ahadi ni YETU.

Siku hiyo imefika, Bibi-arusi anaamini kila Neno naye analitendea kazi. Tumejiweka wenyewe tayari kwa kulisikia na kuliadini Neno Lake.

Kama unahitaji chochote, kama unataka kujazwa na Roho Mtakatifu, kama unataka kuponywa, kama unataka kila pepo atolewe, kama unataka kuwa Bibi-arusi wa Kristo, huu ndio wakati, kuisikia na kuiadini Sauti Yake ndio mahali penyewe.

Ikiwa una haja ya mambo haya na unataka kuwa katika uwepo wa Bwana, karibu zaidi kuliko ulivyowahi kuwa, njoo uungane nasi Jumapili saa 06:00 MCHANA, masaa ya Jeffersonville, [ni saa 1:00 JIONI ya Afrika mashariki–Mh] wakati Jenerali wetu mwenye nyota nne anapomwelekeza Bibi-arusi Mikaya Wake mwenye nguvu jinsi ya kumshinda kila pepo, kila adui, kuwekwa huru, na kujazwa na Roho Wake Mtakatifu, na kuwa tayari kwa ajili ya Kuja Kwake hivi karibuni.

Ndugu Joseph Branham

Ujumbe: *Vita Vikuu Sana Vilivyowahi Kupiganwa. 62-0311*

Maandiko:

1 Petro 5: 8-10

Waefeso 6:10-17

Danieli 12: 1-7